# KUELEWA AMRI

## KATIKA AGANO JIPYA

Inashangaza kama inavyoweza kuonekana kuwa wengi wanafundisha kwamba amri zilizoandikwa na Mungu zimetupuliwa mbali na Kristo. “Kristo alitukomboa katika laana ya torati” (Wagalatia 3:13). Imesemwa pia kuwa sheria imenyakuliwa kabisa na neema na sasa tumewekwa huru kutoka kwa sheria na maagizo zake. Je, hivi ndivyo Biblia inavyofunua kwa kweli?

Ni kweli kwa hakika kwamba hatuwezi kupata wokovu kwa kutii amri. “Hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria” (Wagalatia 2:16), sababu ya msingi ni kwamba hakuna mtu yeyote isipokuwa Bwana Yesu aliyewahi kushika au aliyeweza kutii amri zote kikamilifu. “Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila atajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote.” (Yakobo 2:10).

Wakati ni wazi kuwa hatuko chini ya amri, sheria inafunua utakatifu wa Mungu, haswa amri kumi ambazo zinahusika katika nakala hii. Kwa hivyo, wakati tunaweza kosa kuwa chini ya “amri ya Musa,” tuko chini ya “amri za Kristo”(Wagalatia 6:2).

Katika Yohana 13:34, Yesu alisema, “Amri mpya nawapa, mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo.” Kupenda wengine haikuwa amri mpya, lakini kupenda wengine kama Kristo alivyopenda wengine ni mabadiliko. Hii haikuwa amri pekee

tuliyopewa na Yesu; alitoa maagizo maalum ya mafundisho mengi ya kutufundisha jinsi ya kujibu na kuonyesha aina yake ya upendo. Sasa tunapaswa kuwapenda wenzetu kulingana na upendo wa kujitolea wa Yesu kwetu. Upendo wa Yesu utaleta wale hawana imani kwake na kuweka walio na imani kuwa na nguvu na umoja katika ulimwengu unaompinga Mungu. Ni lazima tuige mfano wa Yesu. “Mkinipenda, mtazishika amri zangu”(Yohana 14:15).

Ibada za kutoa – dhabihu za sheria ya Musa, bila shaka, hazihitajiki kwetu tangu kifo na ufufuo wa Kristo. Dhabihu ya wanyama, ukuhani unaoongoza, na sheria zote za ibada hazihitajiki sasa. “Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa” Wahebrania 10:14

Ni muhimu sana kwamba hadi sasa Amri Kumi zimerudiwa katika Agano Jipya ili kueleza mapenzi ya Mungu kwa waumini wa kikristo, sio kama hali ya wokovu lakini kama mwenendo halisi ya mkristo, na njia mpya ya maisha.

**Marudio ya Amri Kumi**

Haiwezekani kwa waumini wa kweli wa kikristo kuwacha maisha ya kikristo bila ya kushika amri kumi kwa sababu ifuatayo .

Kutoka 20:1-2: “Mungu akanena maneno haya yote akasema, mimi ni Bwana, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa.”

**Amri ya Kwanza:** “Usiwe na Miungu mingine ila mimi” (mstari 3).

**Amri ya Agano Jipya**: “Nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako yote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote” (Marko 12:30).

Wakati Yesu alitaja Amri ya kwanza katika agano jipya, alikuwa wazi kuwa tunapaswa kuweka Mungu kwanza katika kila kitu na kumpenda kwa moyo wetu wote, roho yetu yote, akili zetu zote na kwa nguvu zetu zote. Wakati Shetani anaweza kuridhika kwa kipande cha roho yetu, Mungu Baba yetu anataka roho yetu nzima, sio kipande tu.

Angalia kiwango Mtume Paulo alifikia ili kuonyesha upendo wa Mungu wa kweli katika 1Wakorintho 13. "Upendo huvumulia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahi udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumuliya yote; huamini yote; hatumaini yote; hustahimili yote." (1 Wakorintho 13: 4-8).

Jamii ya kisasa haujui kutofautisha upendo na tamaa. Upendo wa Mungu huelekezwa kwa wengine, sio kwetu wenyewe. Upendo wa Mungu sio la kichoyo. Upendo wa Mungu sio la kwaida kwetu. Inawezekana tu ikiwa Mungu atatusaidia kuweka kando matarajio zetu, ili tuweze kupendana bila ya kutajiria chochote kama malipo.

**Amri ya Pili:** "Usijifanyie sanamu ya kuchongwa, wala mfano wa kitu chochote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana waouvu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu wanipendao, na kuzishika amri zangu" (Kutoka 20:4-6)

**Amri ya Agano Jipya:** Mtume Paulo aliweka wazi juu ya yale ambayo sisi wakristo wa Agano Jipya hatupaswi kufanya. "Wala msiwe waabudu sanamu kama wengine wao walivyokuwa: Kama ilivyoandikwa, watu waliketi kukula na kunya na kusujudu miungu za kipagani. Hatupaswi kufanya usherati kama wengine wao walivyofanya,

wakaanguka siku moja watu ishirini na tatu elfu. Wala tusimjaribu Bwana kama wengine wao walvyomjaribu, wakaharibiwa na nyoka. Wala msinung'unike, kama wengine wao walivyo nung'unika, wakaharibiwa na mharabu.(1Wakorintho 10:7-10).

Hasa katika barua za Paulo, ibada ya sanamu hutumika kwa kujitolea kwa mtu kwa dhamana yoyote isipokuwa kwa Yesu Kristo kama Bwana. Katika Warumi 1:18-32, ni dhahiri kwamba ibada ya sanamu kwa ujumla kulingana na Paulo ni kuweka mapenzi ya kibinafsi mbele kabla ya kumtukuza na kumtumikia Mungu. "Hakuna mtu anayeweza kuwatumikia mabwana wawili," (Mathayo 6:24)

**Amri ya tatu:** "Usilitaje bure jina la Bwana, Mungu wako, maana Bwana hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajae jina lake bure" (Kutoka 20:7).

**Amri ya Agano Jipya:** Kuhusu amri hii ya tatu Yesu alisema, "Lakini mimi nawaambia, usiape kabisa; hata kwa mbingu, kwa maana ndicho kiti cha enzi cha Mungu: wala kwa nchi, kwa maana ndio pa kuwekea miguu yake; wala kwa Yerusalemu, kwa maana ndio mji wa falme mkuu.Wala usiape kwa kichwa chako, maana huwezi kufanya unywele mmoja kuwa mweupe au mweusi" (Mathayo 5:34-36).

Katika ukweli wa ulimwengu wa sasa ni nadra sana kwamba watu wanafikiria wanahitaji kuweka kutilia maneno zao kwa viapo, ahadi, matusi, na wakati mwingine huchukua jina la Mungu bure. Inatarajiwa kwa wakristo kwamba watasema ukweli. Hivyo haihitajiki kutoa kiapo au ahadi. Yakobo aliandika, "Lakini zaidi ya yote, ndugu zangu, msiape, wala kwa mbingu wala kwa nchi; wala kwa kiapo kiinginecho chote; bali ndiyo yenu na iwe ndiyo na sio yenu iwe sio, msije mkaangukia hukumu" (Yakobo 5:12). Kwa kuzuia uwongo, ukweli wa nusu, na kuachana na ukweli, tutajulikana kama watu wanao aminika.

**Amri ya nne:** “Ikumbuke siku ya sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo tusifanye kazi yoyote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya mlango yako. Maana, kwa siku sita Bwana alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo bwana akaibariki siku ya sabato akaitakasa.” (Kutoka 20:8-11).

**Amri ya Agano Jipya:** Kulingana na Yesu, sabato ilitengenezwa kwa wanadamu wote, sio Wayahudi tu. “Akawaambia, sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato. Basi Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato pia” (Marko 2:27-28).

Kwa mafarisayo, sheria za sabato zilikuwa muhimu zaidi kuliko mapumziko ya sabato. Yesu alielewa kuwa kusudi ya sheria za Mungu ni kukuza upendo kwa Mungu na watu wengine, na kuifanya sabato kuwa ya kupendeza.

Katika waebranea 4:8-11, Paulo anaandika, “Maana kama Yoshua angaliwapa raha, asingali nena siku ingine baadaye. Basi, imesalia mapumziko ya sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi yake, basi, na tufanye bidii kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu yeyote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi.”

Yesu ametupatia pumziko letu kwa njia ya imani. Hatufai kufanya kazi. Hilo sio kupambana kwa kazi nzuri ili kupata wokovu . Inarejelea kufanya kila juhudi kupata kile Mungu ametoa. Haifai kuchukuliwa kama mzaha. Inahitaji uamuzi wa kujitolea kustahili mapumziko ambayo Mungu ametoa. Ikiwa tutaweza kuingia katika pumziko la

Mungu lazima tuamini kuwa Mungu ana uhusiano kati yetu. Tunapaswa kumtegemea Yesu kutuletea pumziko la Mungu, na kuamua kumfuata kwa utiifu.

Katika Agano Jipya, kwa mshangao wa wengi, Yesu na mitume hawakushika tu sabato ya siku ya saba lakini pia siku zote takatifu za Mungu, ambazo huchukuliwa kuwa siku za sabato pia. Kisha Bwana akamwambia Musa, "Nena na wana wa Israeli, nakuwaambia, siku kuu za Bwana, ambazo mtazipigia mbiu kuwa ni makusanyiko matakatifu; hizi ni siku kuu zangu" (Mambo ya Walawi 23:1-2).

Vifungu vifuatavyo katika Agano Jipya vinaonyesha wazi kuwa Yesu na mitume wake walishika siku zote kuu na makusanyiko matakatifu za Mungu:

Luka 2:41-42: "Basi, wazee wake huenda Yerusalemu kila mwaka, wakati wa *siku kuu ya pasaka*. Na alipopata umri wake kumi na miwili, walipanda kama ilivyo desturi ya siku kuu; na walipokwisha kuzitimiza siku, wakati wa kurudi kwao, Yule mtoto Yesu alibaki nyuma huko Yerusalemu, na wazee wake walikuwa hawana habari."

Yohana 7:2: "Na siku kuu ya Wayahudi, siku ya vibanda, ilikuwa karibu. Basi ndugu zake wakamwambia, ondoka hapa, uende Uyahudi, wanafunzi wako nao wapate kuzitazama kazi zako unazozifanya."

Yohana 7:37: "Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya siku kuu, Yesu akasimama, akapaza sauti yake akasema, Mtu akiona kiu na aje kwangu anywe."

Matendo 12:3 : "na akiona ya kuwa imewapendeza Wayahudi akaendelea akamshika na Petro. Siku hizo zilikuwa siku za mkate isiyo chachu."

Matendo 20:6 : “Sisi tukatweka baada ya siku ya mkate isiyotiwa chachu, tukatoka Filipi.”

Matendo 20:16 : Kwa sababu Paulo amekusaidia kupita Efeso merikebuni, asije akakawahi katika Asia; kwa maana alikuwa na haraka, akitaka kuwahi Yerusalemu siku ya pentekoste, kama ikiwezekana.”

Matendo 27:9 : “Na wakati mwingi ulipokwisha kupita na safari ikiwa ina hatari sana, kwa sababu siku za kufunga zilikuwa zimekwisha kupita (hiyo ni siku ya upatanisho),”

1 Wakorintho 5:6-8: “Kujisifu kwenu si kuzuri. Hamjui kwamba chachu kidogo hulichachusha donge zima? Basi jisafisheni, mkatoe ile chachu ya kale, mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo hamkutiliwa chachu. Kwa maana pasaka wetu amekwisha kutolewa kwa sadaka, yaani, Kristo; basi na tuifanye karamu, si kwa chachu ya kale wala kwa chachu ya uovu na ubaya bali kwa yasiyochachika, ndio weupe wa moyo na kweli.”

1 Wakorintho 16:8: “Lakini nitakaa Efeso hata pentekoste.”

Si vibaya kudhani kwamba siku za siku kuu za kila mwaka zinamalizika kwa dhabihu ya Kristo, kwa sababu tu walikuwa wameunganishwa na mfumo ya dhabihu ya hekalu. Madhumuni ya siku ya karamu ya Mungu hayadhibitiwi na mfumo wa dhabihu, lakini kwa kile wanachoelekeza. Ikiwa karamu zilikuwa zimeelezea ukamilifu ya ukombozi wa kukuja kwa Kristo ya kwanza, basi kazi zao zingekuwa zimekomeshwa wakati wa kusulubiwa. Walakini, ikiwa siku kuu hiyo inadhihirisha pia ulaji wa ukombozi wa kutimizwa na Kristo wakati wa ujio wa pili, basi kazi hiyo inaendelea katika kanisa la kikristo na maana mpya na njia ya maadhimisho. Siku takatifu za Mungu zinaonyesha wazi mpango wake wa ukombozi na upatanisho kutoka mwanzo hadi mwisho.

**Amri ya tano: “**Waheshimu Baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako.” (Kutoka 20:12)

**Amri ya Agano Jipya:** “Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. Waheshimu baba yako na mama yako – hii ndio amri ya kwanza yenye ahadi – upate heri, ukae siku nyingi katika Dunia” (Waefeso 6:1-3)

Kutii inamaanisha kufanya jinsi ulivyoagizwa. Kuheshimu inamaanisha heshima na upendo. Hii itatokea ikiwa wazazi na watoto wataweka masilahi ya wengine juu ya yao, ni kwamba, ikiwa “wanatiana.”

**Amri ya sita:** “Usiue” (Kutoka 20:13)

**Amri ya Agano Jipya:** “Maana mtu wa kwenu asiteswe kama mwuaji au mwizi, au mtenda mabaya au kama mtu ajishughulisaye na mambo ya watu wengine” (1 Peter 4:15).

Sio aibu kwetu kuteseka kuwa mkristo, na tukifanya hivyo tunaweza kuwa na hakika, Yesu atakuwa nasi kwa njia yote. “Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni” (Mathayo 5:16).

**Amri ya saba:** “Usizini” (Kutoka 20:14)

**Amri ya Agano Jipya:** “Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu.” (Waebrania 13:4).Wakristo lazima wawe na heshima kubwa kwa viapo vyao vya ndoa. Upendo kati ya mume na mke lazima ulelewe kwa maisha ya kupendeza. Mwenzi wa ndoa lazima ahakikishe kwamba upendo wao unaendelea sana kuathiri vizuri ukarimu wao, huruma, uaminifu, na kurithika.

**Amri ya nane:** "Usiibe" (Kutoka 20 :15).

**Amri ya Agano Jipya:** "Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi akitenda kazi hiyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawiya mhitaji" (Waefeso: 4:28).

**Amri ya tisa:** "Usimsuhudie jirani yako uwongo" (Kutoka 20:16).

**Amri ya Agano Jipya:** "Msiambiane uwongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake; mkivaa utu mpya, unaofanywa upya upate ufahamu sawa sawa na mfano wake yeye aliyekuumba." (Wakolosai 3:9). Ikiwa tutasema uwongo kati yetu itasumbua umoja katika maisha ya kibinafsi, kuharibu kuaminiana, kuvunja uhusiano na kusababisha mgawanyiko kanisani. Kama Wakristo tuko kwenye mwendelezo wa maendeleo ya elimu. Kadiri tunavyojuwa na kuelewa juu ya Yesu Kristo na kazi zake ndivyo tunabadilishwa kuwa kama Yeye. Hatupaswi kamwe kuwacha kujifunza na kumtii Yesu au turuhusu twende tu. Kuna motisha kubwa ya kupata hazina kubwa ya kukuwa ndani yake, "Yote ikiwa ni umilele."

**Amri ya Kumi: "**Usitamani nyumba ya jirani yako, usitamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala chochote alicho nacho jirani yako" (Kutoka 20:17).

**Amri ya Agano Jipya:** "Maana neno hili mnalijua hakika, ya kwamba mwasherati, wala mchafu, wala mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu aliye na urithi katika ufalme wa Kristo na Mungu." (Waefeso 5:5). Ufanisi, zaidi ya umaskini, unaweza kufifisha maono yetu ya kiroho kwa sababu hutuelekeza kufanya tuwe wa kutosha kwa hamu ya kupata zaidi ya kila kitu, isipokuwa Mungu.

“Vita vyatoka wapi, na mapigano yalioko kati yenu yalitoka wapi? Si humu, katika tamaa zenu zifanyazo vita katika viungo vyenu? Mwatamani, wala hamna kitu, mwaua na kuona wivu, wala hamwezi kupata. Mwafanya vita na kupigana, wala hamna kitu kwa kuwa hamwombi! Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu” (Yakobo 4:1-3).

Kama vile chuki inasababisha kuuawa, vivyo hivyo uchoyo husababisha ugomvi na tamaa ya uzinzi.

**Je! Sheria ya Mungu imekamilika?**

Hapana! Kwa kweli sheria ya Mungu haijakamilika. Ni kama vile Yesu alisema, “Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiza” (Mathayo 5:17). Yesu aliongeza sheria na kuifanya iheshimiwe.

Je! Paulo alimaanisha nini aliposema” Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, amelaaniwa kila mtu aangikwae juu ya mti” (wagalatia 3:13)? Sheria yenyewe sio laana; na amri ya mungu sio ngumu. Yohana anatueleza, “kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito ” (1 Yohana 5:3).

Laana ya sheria ni adhabu ya kifo iliyo juu yetu.Yesu kwa kubeba dhambi zetu msalabani, alichukuwa dhambi zetu na kuondoa adhabu ya kifo kwetu ambayo hatukungeweza kugharamia. “Yeye mwenyewe alizichukuwa dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi tuwe hai, kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake tuliponywa”(1 Petro 2:24).

**Hitimisho**

Swali ambalo lazima tuulize sasa ni, ni nini kilisulubiwa msalabani?

Ni wazi kwamba Kristo ndiye aliyesulubishwa kwa msalaba. Ni yeye ndiye aliyebeba dhambi zetu. Alimwaga damu yake kutoka msalabani kwa ajili yetu, alifuta dhambi zetu zote kupitia maisha yake mwenyewe. Ni dhambi ambayo ilifutwa. "Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe" (Matendo 3:19). "Ee Mungu, unirehemu," Daudi alilia, "uyafute makosa yangu" (Zaburi 51:1,9).

Angalia taarifa hii nzito. "Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya" (2 wakorintho 5:10). Je! Damu ya Kristo hufunika dhambi zetu zote? Je! Dhambi zilizosimama dhidi yetu zimefutwa?

Badilika sasa kwa ufunuo wa Ufunuo 20:12, na uone kile kinachotendeka katika hukumu ya mwisho. "Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya kiti hicho cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu waka hukumiwa katika mambo hayo yaliyoandndikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao"

Mstari huu unaonyesha wazi kuwa rekodi ipo iliyo na dhambi zote ambazo ni dhidi yetu.Tutahukumiwa ipasavyo, isipokuwa damu ya kristo inazifunika au kuzifuta. Kristo alikufa ili kufuta rekodi iliyoandikwa ya dhambi zetu za hatia. Rekodi ya dhambi zetu za zamani imetiwa msalabani, imeondolewa njiani, na kumalizika kabisa. Kwa hivyo, tunaweza kuwa na hakika kuwa maagizo na dhambi ambazo zilikuwa dhidi yetu zimefutwa. Na sio sheria ya Mungu wala amri zake.

Walimu wengi wa uongo wa karne ya kwanza walifundisha kwamba wakristo wanaweza kufanya chochote wanataka na kuishi maisha yao kwa njia yeyote ile waliochagua bila kuogopa adhabu ya Mungu. Yuda

alionya dhidi mwenendo kama huo. “Kwa maana kuna watu waliojiingiza kwa siri, watu walioandikiwa tangu zamani hukumu hii, makafiri, wabadilio neema ya mungu wetu kuwa ufisadi, nao humkana yeye aliye peke yake Mola, na Bwana wetu Yesu kristo” (Yuda 1:4)

Ujasusi inamaanisha kuishi maishi yako katika makusudi, machafuko, na njia mbaya. Waliishi maisha ya ujasusi kwa sababu waliamini neema ya Mungu imewapa uhuru wa kufanya wanavyotaka na kugeuza neema ya ajabu ya Mungu kuwa ujasusi.

Agano jipya inasema kwa uwazi kuhusu amri za “Agano ya kale” na inatufunza kwamba wataonyesha mapenzi ya Mungu kwa ukristo.” Kwa hivyo, sheria ni takatifu, na amri ni takatifu, ni haki na nzuri kwa kuwa ndani yangu nafurahia sheria ya Mungu” (Warumi 7:12-22).

Kwa hivyo, kama wakristo tupaswa kupenda na kutii amri za Mungu sio kwasababu kufanya hivyo kunatuokowa lakini kwasababu tumeokolewa kwa neema kupitia imani katika zawadi ya Mungu ya upendo katika Kristo, aliybeba dhambi zetu msalabani. “Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa kata uzima wake” (Warumi 5:10).